# Standard 8 End Term 1 Exam, 2016

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

Tumia penseli ya kawaida.

Hakikisha umeandika kwa karatasi yako:

(i) JINA LAKO (iii) JINA LA SHULE YAKO

Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora mstari kwenye herufi uliyopewa

**oma kifungu kifuatavyo. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu faalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Ukimwi ni ugonjwa _____1_____ na tabia za kujamiana. Jambo hili limekuwa tatizo katika _____2_____ nyingi za dunia. mma unaoishi mahali _____3_____ hakupatikani maadili na utu huwa _____4_____ nguvu za kuangamiza, _____5_____ za ızuilia gonjwa hili. Kwingineko tatizo huwa la kutopata maarifa ya kukinga mwili kutokana na janga hili. Katika hali ımna _____6_____ suluhisho ni kuelimisha watu _____7_____ ya kujikinga kwani kinga ni bora kuliko tiba.

Siku hiyo aliamka _____8_____. Baada ya kiamshakinywa alishika kifurushi chake _____9_____ kwapani. Baadaye _____10_____ chache hadi barabara kuu. Kufika hapo akaona _____11_____ nchi ilivyokuwa tambarare ıdi _____12_____ wa macho yake. Akashika barabara, _____13_____ basi safari _____14_____ ikawa _____15_____.

| | | | |
|---|---|---|---|
| A. unaosababisha | B. unaosababishia | C. unaosababishwa | D. unaosababishana |
| A. pembe | B. kuta | C. bahari | D. nyumba |
| A. ambapo | B. ambamo | C. ambalo | D. ambako |
| A. hauna | B. hakuna | C. hawana | D. haina |
| A. ila | B. wala | C. bali | D. ili |
| A. hizi | B. hili | C. hivi | D. hii |
| A. mbinu | B. harakati | C. jinsi | D. hatua |
| A. alfajiri | B. adhuhuri | C. alasiri | D. jioni |
| A. akakitwika | B. akakieleka | C. akakitia | D. akakikimbatwa |
| A. akapiga hatua | B. akafanya hatua | C. akachukua hatua | D. akafunga hatua |
| A. kwamba | B. jinsi | C. sababu | D. ambayo |
| A. uzuri | B. upeo | C. ukali | D. ukubwa |
| A. hivyo | B. hiyo | C. huo | D. huu |
| A. yao | B. yake | C. zake | D. zao |
| A. imeanza | B. kimeanza | C. limeanza | D. wameanza |

**Kutoka swali la 16 - 30, chagua jibu mwafaka**

16. Maria alinunua mkeka uliofumwa vyema kutoka kwa ___
   A. mfumaji  B. msusi
   C. mfumi  D. mtarizi
17. Babuye chineda alimwona chui, mbuzi wake wakasalimika. Kwa hivyo tutaenda kumpa ______
   A. mkono wa tahania  B. mkono wa buriani
   C. mkono wa tanzia  D. mkono wa huruma
18. **Ki - imetumikaje katika sentensi hii:**
   Mweni alipokuja alinipata nikilala.
   A. hali ya masharti  B. hali ya kumithilisha
   C. hali ya kuendelea  D. hali ya udogo
19. Pole pole, vibaya, alasiri, njiani, ni aina ya ______
   A. vielezi  B. vivumishi
   C. nomino  D. viwakilishi
20. Kivumishi cha sifa kutokana na kitenzi angaa ni__
   A. mwanga  B. mwangaza
   C. angavu  D. mwangao
21. Nomino **habari** iko katika ngeli lipi?
   A. U-ZI  B. I - I
   C. U - I  D. I - ZI
22. Tano ni kwa chokaa kama vile kitita ni kwa ____
   A. pesa  B. funguo  C. ndizi  D. kuni
23. Kinda ni kwa ndege ilhali ______ ni kwa chungu.
   A. king'ovyo  B. kichuguu
   C. bobwe  D. kwida
24. Asingalienda kwake asubuhi asingalimkuta. Inamaanisha
   A. Hakuenda kwake asubuhi lakini alimkuta.
   B. Alienda kwake asubuhi lakini hakumkuta.
   C. Alienda kwake asubuhi wala hakumkuta
   D. Hakwenda kwake asubuhi waka hakumkuta
25. Methali inayotufunza kuwa jambo linaloonekana zito kwa mwingine laweza kuwa rahisi kwako ni ______
   A. Bahati ya mwenziyo usiilalie mlango wazi
   B. Mzigo wa mwenzio, ni kanda la usufi
   C. Kila mwamba ngoma huvuta kwake
   D. Kwako kukiungua kwa mwenzio kwateketea
26. Tumia kiunganishi mwafaka: Iwe vitini ______ chini sisi tutakaa.
   A. pia  B. na  C. au  D. kwa
27. Lali na Lola ______ kwa sababu ya nyumba.
   A. wanachapta  B. wanachapana
   C. wanachapisha  D. wanachapa
28. Chagua kisawe cha neno lililopigwa mstari
   Nguo yake ilikuwa na **mapaku** meusi na meupe.
   A. mistari  B. madoa
   C. michoro  D. nakshi
29. Tambua kinyume cha neno lililopigwa mstari kwenye sentensi.
   Mtu yule **fakiri** amebwaga zani.
   A. mjinga  B. fukara
   C. maskini  D. mkwasi
30. Tia mapambo katika kitu ili kipendeze machoni ni ______
   A. rembesha  B. rembo
   C. kupamba  D. remba

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40**

Wewe umewahi kusikia kuwa ugonjwa fulani umefunga safari kumtafuta mtu au binadamu umushike au kumdhuru. Umewahi kukutana na gonjwa lolote likiabiri matwana au shangingi ati linaenda kumvamia bwana fulani au bibi fulani? Kama umewahi basi heri jibari na uniache na ujuha wangu. Nimechajua ni kuwa aghalabu waja ndio hutafuta ugonjwa kwa kutia pamba masikioni. Kila mmoja anastahili **kujibari** ndio kwani likikushika! Hatima yako itakuwa kufarakana na dunia.

Kila siku redio yavuna na kutangaza kwamba nawa mkono kabla ya kula au baada ya kutoka msalani. Tumia sabuni fulani kujikinga na viini vya bakteria. Unapolala, lala ndani ya chandarua kilichotiwa dawa ili usiumwe na mbu. Tumia dawa fulani kuua wadudu, usivute sigara, usiinywe pombe wala kutumia dawa yoyote ya kulevya, usile chakula kilicho na mafuta mengi, usitumie sukari nyingi, tumia kinga ukifanya mapenzi na mengine. Wewe wajifanya sugu, hamnazo usiyesikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Huambiliki husemezeki. Wataka kuhisi utamu wa mambo kwa muda mfupi wa dakika kadha kisha ubaki na machungu ya milele. Hata sasa unaambiwa maneno ya busara, fungua roho yako ongea, fanya hiyo hesabu, wacha mpango wa kando, 'nimechil' na kadhalika. Sisi wenyewe twajiangamiza. Twajifisha kwa hiari. Hata tukipewa dawa hatumezi ili tupone. Shauri lako.

Furaha yangu ni kuwa nduli huyu wa Ukimwi hawezi kukupata kwa kumsalimia, kumpiga pambaja au kuketi na mja aliye nao. Njia ambayo kwa asilimia kubwa huueneza ugonjwa huu ni ngono ya ovyo ovyo huku ukijitia hamnazo. Mara kwa mara utawakuta vijana wadogo wana vimwana. Hata unashindwa wanaambiana nini katika maongezi yao. La ibra pia ni pale unapoyakuta majibaba yaliyokula yakashiba, yenye matumbo makubwa kama viriba yakihusiana kimapenzi na vigori ati ndivyo vilivyo salama!

Eti wanajali mabikira na licha ya hayo hawana virusi vya ukimwi. Nani kawaaambia kuwa yote yang'aayo ni dhahabu! Hawajui kuwa <u>uzuri wa kuyu ndani mabuu</u>?

Akina mama nao twiwatie maamumu. Mbona waitwe waali ilhali hao ndio wanaoing'ang'ana wakembe wadogo bila haya wala aibu? Mara ngapi tumesikia kuwa janajike linakwamilia kijivulana kidogo eti ndicho mume? Ukiuliza utaambiwa kuwa wakubwa wanaugua maradhi yasiyo na uganga. Linalokera zaidi ni kuwa aghalabu watu hawa wanaopenda mambo ya ukwate haramusi ati wana mpenzi mmoja! La! Wanasema kuwa na mpenzi mmoja ni kujishusha hadhi. Utakuta ana kimwana katika kila mji. Mmoja Nairobi, mwengine Kisumu, mwengine Mombasa, mwengine Nakuru na pengi penginepo!

Kwa kweli kama huko ndiko kupnda raha jinsi wengine wanavyodai, basi sina haja wala raghba ya kufurahia maishani. Ati penda raha kufa kwaja? Adinasi razini anaweza kusoma hivyo hasa katika kizazi hiki? kueneza ukimwi kusiwe lengo letu kwani mshahara wa tabia mbi kama hiyo ni mauko ya aibu.

31. Kwa mujibu wa aya ya kwanza ________
   A. ugonjwa humtafuta mtu
   B. mahuluki wengi hujitakia janga la ugonjwa fulani
   C. watu huugua kwa bahati mbaya
   D. ni mhali watu kuugua ovyo ovyo

32. Neno **kujibari** lina maana kuwa:______
   A. tujichunge B. tujizatiti
   C. tujhimize D. tujitenge

33. Ni jambo lipi linalomfariji mwandishi huyu?____
   A. kufahamu kuwa ukimwi haumpati mtu kwa kumkaribia tu aliyeathiriwa
   B. maradhi mengi yana tiba
   C. watu hufunga ndoa baada ya kupimwa
   D. ni vigumu kupata ukimwi mkijamiana

34. Ni nini maana ya kumpiga mtu pambaja?_____
   A. kumpiga mapaja B. kumkaribia
   C. kumkumbatia D. kumpa nasaha

35. Ukweli ni kwamba ________________
   A. Asilimia ndogo haienezi ukimwi
   B. Uhusiano mwingi wa kimahaba hufanywa isivyostahili
   C. Waja wengi wanazingatia maadili
   D. Haipo haja ya kupigana dhidi ya ukimwi

36. Ni sababu gani inayotolewa na wale wanaowahushisha vijana wadogo katika mambo ya mapenzi?______
   A. wengi hudhani vijana hawapo katika hatari hiyo kama waliokwisha komaa
   B. ni kawaida ya kizazi cha karne hii
   C. wengi hawajali matokeo ya baadaye
   D. wengi huo ndio uraibu wao hasa

37. Ni methali gani inayokaribiana kimaana na iliyopigwa mstari?_______
   A. Ganga ganga za mganga humuacha mgonjwa na matumaini
   B. Uzuri wa mkakasi ndani pande la mti
   C. Visima vya kale havifukiwi
   D. Vyanda vya miguu havivishi pete

38. Ni nini hasa kinachochangia kueneza ukimwi kwa mujibu wa habari hii?_____
   A. Kufanya mapenzi bila kutumia kinga
   B. Kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja hasa wakati umevipata virusi
   C. Kushirikiana kimapenzi baina ya wazee na vijana
   D. kuponda raha kupita kiasi

39. Mwandishi anamalizia kwa kutoa wasia upi?____
   A. Heri kutoponda raha kama hatima yake ni mauti
   B. Heri tuponde raha kwani kufa kwaja
   C. Tuhimize wanaohusiana kimapenzi
   D. Dhamira ya kueneza ukimwi itimizwe

40. Kichwa gani kinachofaa habari hii?
   A. Wazee, vijana na ukimwi
   B. Tabia za kufana
   C. Wasichana mabikira
   D. Uozo wa maadili

**<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50</u>**

Hamisi alikuwa mtoto jeuri sona katika kijiji chao. Watu wengi walilalamika kwa wazazi wake kwamba tabia ya Hamisi ilikuwa mbaya. Baba na mama yake Hamisi hawakujali. Kila siku alipotoka shuleni, Hamisi alikwenda kwenye mashamba ya jirani kuiba miwa.

Watoto wengi walifuatana na Hamisi kwa sababu yeye hakuogopa kuwaibia vitu vya watu mashambani. Hamisi akishaiba huwagawia watoto hao wakala na kumsifu kwamba alikuwa hodari. Hamisi alipenda sifa. Alifurahi sana aliposifiwa na kuendelea

na wizi. Ingawa hawakuwa wezi, walimpa kichwa mwenzao akaendela sifa. Shuleni, walimu walimfundua kuwa mtoto mtukutu Walimu walichunguza chochote alichokitenda kwa makini na kuwaadhibu vikali. Kwa hivyo, hakudiriki kufanya ukorofi shuleni Alingojea mpaka wakati wa kwenda nyumbani.

Siku moja, Hamisi na wafuasi wake watano walikwenda kutembea ng'ambo ya mto uliopita karibu na kijiji chao. Ng'ambo ya mto kulikuwa na mashamba ya ndizi, kahawa, machungwa na mapera. Walipofika kwenye kivuko cha mto walianza kuvuka. Katika mto walipishana na mzee mmoja aliyekuwa amebeba mkunga wa ndizi. Yule mzee alitoka shambani akiwa na mizigo miwili, mkungu wa ndizi na bahasha ya machungwa ng'ambo ya mto, akarusha mkunga wa ndizi kwanza.

Watoto walifika ng'ambo na kuona bahasha ya machungwa. Mara Hamisi akawaambia wenzake waibe bahasha wakimbie nayo. Wenzake walisema wanamuogopa yule babu na wakakataa kuiba. Hamisi aliiba machungwa. Walimueleza jinsi mwenzao alivyoiba mchungwa. Mzee alicheka na akawaambia wachukue kila mmoja wao chungwa moja moja kwa sababu walionyesha hulka njema.

Hamisi alikimba mpaka kwenye jiwe kubwa akaketi na kula machungwa yote. Alipofika nyumbani tumbo lake lilianza kuvimba na akawa na maumivu sana. Aliogopa na akawaambia wavyele wake.

Walijaribu kumpeleka kwa madaktari lakini hakupona. Baadaye walimpeleka kwa mganga aliyewaambia waende wakamtake radhi huyo mtu aliyemuibia. Walishindwa kumpata huku tumbo la Hamisi likiendelea na kuwa jekundu. Baada ya muda, tumbo lake lilipasuka na kutoa machungwa kumi. Alipokata kamba na kuwaacha wazazi wake kwa majonzi na simanzi.

41. Ni kwa nini watu wa Karia walilalamika?
A. Hamisi aliiba machungwa ya mzee
B. Hamisi hakupenda kwenda shule
C. Hamisi aliwafundisha wenzake wizi
D. Hamisi alikuwa na hulka borongo

42. Katika kivuko, Hamisi na wenzake__________
A. waliona matunda ng'ambo ya pili
B. walikutana na shaibu
C. walikutana na mzee akibeba machungwa
D. walikutana mzee akiwa na mizigo miwili

43. Jambo lililomfanya mzee kuacha machungwa ng'ambo ya mto lilikuwa
A. alitaka watoto wamsaidie kuyavusha
B. hakuweza kuvusha mizigo yote pamoja
C. hakujua alikuwepo mwizi kati ya wale watoto
D. hakuweza kuvusha mizigo miwili pamoja

44. Hamisi **hakudiriki** kufanya ukorofi shuleni inamaanisha?
A. hakuogopa
B. hakupenda kufanya ukorofi
C. hakupiga mshipa
D. hakuwa akifanya ukorofi

45. Ni nini kilichomzuia Hamisi kufanya ukorofi shuleni?
A. aliadhibiwa vikali
B. aliogopa wavyele wake
C. alikosa cha kuiba
D. alifukuzwa shuleni

46. Ghulamu hawa walikuwa wanaenda ng'ambo ya mto _____
A. kuona mzee na shamba lake
B. kufundishwa wizi
C. matembezi
D. kuiba machungwa

47. Kwa nini watoto waliogopa kumfuata mwenzao?
A. waliogopa yule shaibu
B. walitaka kuomba machungwa
C. alichana mbuga bila wao kujua
D. aliwakanya wasimfuate

48. Babake Hamisi alikwenda kwa mganga kwa kusudi la _______
A. kumtafuta mzee mwenye machungwa
B. kupiga ramli na kumroga mzee mwenye machungwa
C. kulipa yule mzee machungwa yake
D. kupiga ramli na kumponya mwanawe

49. Unafikiri ni kwa nini mzee alicheka alipoambiwa jinsi Hamisi alivyofanya?
A. Aliwahurumia watoto hao kwa kutoiba
B. Alikuwa anajua fika jambo litakalotendeka kwa Hamisi
C. Alikuwa na mpango wa kumuua Hamisi
D. Kulikuwa na wadui kati ya watu wa vijiji

50. Methali ifaayo zaidi kwa hadithi hii ni _______
A. Mwendatezi na omo marejeo ni ngamani
B. Asiyekujua hakuthamini
C. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia
D. Mjinga akierevuka mwerevu yu mashakani